# Wahusika wa Kitashtiti katika *Gamba la Nyoka*

Mwenda Mbatiah


## Ikisiri

*Makala haya yanachunguza uumbaji wa wahusika katika Gamba la Nyoka ambayo ni mojawapo ya riwaya za Euphrase Kezilahabi. Tumewatambulisha wahusika wakuu watano ambao ni Mambosasa, Mamboleo, Padri Madevu, Mama Tinda na Mzee Chilongo. Hawa ndio wahusika ambao tunawachunguza. Lengo letu ni kudhihirisha kwamba uumbaji wa wahusika hawa umetumia mtindo wa kitashtiti. Mbinu za utunzi zinazohusishwa na tashtiti ni kama vile kinaya, ucheshi, dhihaka na bezo. Kwa vile tashtiti hudhamiriwa kukashifu na pia kupiga vita maovu ya kijamii, makala haya yanaangazia matumizi ya mbinu hizi katika kufanikisha lengo hilo.*


## 1.0 Utangulizi

Istilahi ya "tashtiti" imefasiliwa na jarida la *Mulika* (1984:70) kama ifuatavyo: "Aina ya fasihi inayofanya mtu, jambo au kitu kuwa kidogo kwa kutumia dhihaka na bezo." Maelezo haya yanahusu njia mojawapo ya kutumia tashtiti katika fasihi. Yaani uandishi ambapo kazi nzima inaelezeka kama tashtiti. Lakini kuna njia nyingine tofauti ambapo tashtiti hujitokeza kama vipengele vya kimtindo katika kazi ambayo sio tashtiti hasa (Baldick, 2008:299). Mtindo unaotawala katika kazi kama hii unaweza kuwa uhalisia. Hii ndiyo hali tunayoikuta katika riwaya ya *Gamba la Nyoka*.[1] Kimsingi, hii ni riwaya ya kiuhalisia na kisiasa. Inaakisi utekelezaji wa sera za Azimio la Arusha la mwaka wa 1967. Azimio hili lilihusu ujenzi wa ujamaa nchini Tanzania. Mtunzi anatumia vipengele vingi vya tashtiti kulishughulikia suala hili lenye uzito mkubwa katika historia ya Tanzania. Kwa hali hii, riwaya inayohusika inaweza kurejelewa kama kazi ya kitashtiti.

Kabla ya kuchunguza matumizi ya tashtiti katika *Gamba la Nyoka*, ni muhimu kujadili zaidi istilahi hii ili kuweka wazi jinsi tunavyoitumia katika makala haya. Turejelee maelezo ya *Mulika* hapo juu ambapo tunaambiwa kwamba tashtiti hutumia dhihaka na bezo. Hizi ni baadhi tu ya mbinu ambazo tashtiti hutumia ili kufanikisha malengo yake. Nyingine ni kama vile kinaya, ucheshi, tabaini na

[1] Riwaya hii ilichapishwa mara ya kwanza mwaka wa 1979 na Eastern African Publications, Arusha. Toleo linalorejelewa katika makala hii ni la mwaka wa 2006 lililochapishwa na Vide-Muwa, Nairobi.

chuku. Inafaa kuzifasili istilahi hizi zote. Bezo ni maelezo yanayobeza, yaani yanayoshusha hadhi ya mtu au kitu. Cuddon (1999:430) anaeleza kinaya kama mbinu ya utunzi inayohusu hitilafu au kinyume baina ya usemi fulani na maana yake; matendo fulani na matokeo yake; hali inavyoonekana na ukweli halisi. Hivi ni kusema kwamba kuna aina kadha za kinaya. Dhihaka ambayo pia inajulikana kama kinaya cha kiusemi (Wamitila, 2003:80) inamaanisha matumizi ya maneno ambayo ni kinyume cha maana yake hasa. Kwa mfano, unaposema "Saidi ni shujaa" ukimaanisha kwamba ni mwoga. Pia kuna kinaya cha hali ambapo hali au tukio fulani ni kinyume cha matarajio. Kwa mfano, polisi wa trafiki anapokamatwa kwa kuvunja sheria ya barabarani ni hali isiyo ya kutarajiwa. Mwisho, kuna kinaya cha kijaala. Hii ni hali ya mhusika muhimu kukabiliwa na dhiki na adhabu ambazo hana uwezo juu yake – yaani zinazosababishwa na nguvu za kiungu. Hali kama hii ndiyo inayorejelewa kama majaliwa.

Ucheshi ni mbinu nyingine inayohusishwa na tashtiti. Kulingana na Wamitila (2003:246) maana yake ni "uwezo wa kazi ya kifasihi…kusababisha vicheko…ni mbinu mojawapo katika kazi za kitashtiti." Nayo chuku inaelezwa na Mbatiah (2001:6) kama "Tamathali ya usemi inayotumia lugha ya kutilia chumvi kwa madhumuni ya kusisitiza." Tunamalizia maelezo haya kwa kuangalia mbinu ya tabaini. Hii inaweza kuelezwa kama kinyume cha chuku kwa kuwa inatumia maneno ya kudunisha kitu huku maana yake ikiwa ni kinyume cha maneno hayo. Aghalabu mbinu hii hutumia neno "si" la kukanusha. Kwa mfano unaposema "Selemani si mjinga" ukimaanisha kuwa ni mwerevu sana.

Mtindo wa kitashtiti hutumia mbinu zilizotajwa hapo juu na nyingine nyingi kama silaha ya kupigana na maovu ya kijamii na wale wanaohusika nayo. Lengo lake huwa ni kurekebisha hali mbaya za kijamii au tabia za wanaohusika na maovu mbalimbali. Katika makala haya tunachunguza jinsi mbinu hizi zilivyotumiwa katika uumbaji wa wahusika wakuu katika riwaya ya *Gamba la Nyoka*.

## 2.0 Mamboleo na Mambosasa

Hawa ndio wahusika muhimu zaidi riwayani. Yaani ndio waliokuzwa zaidi. Aidha, ndio wanaohusika na matukio na maudhui makuu. Tunawashughulikia kwa pamoja kwa sababu wanalingana kwa mambo mengi. Kwanza, wamekuzwa kwa karibu kiwango sawa. Wana kiwango sawa cha elimu, wamekulia na kuelimishwa katika mazingira sawa na wote wawili wanashiriki katika ujenzi wa ujamaa. Hata majina yao ya kimajazi hayatofautiani sana. Yanadokezea mawazo yao ya kimaendeleo ambayo wanayawakilisha. Mabadiliko yanayohusika ni ya ujenzi wa Tanzania mpya katika misingi ya ujamaa baada ya Azimio la Arusha. Suala hili la kuwamithilisha na mabadiliko ni njia mojawapo ya kufanikisha kuchorwa kwao kitashtiti. Anayechekesha zaidi kati yao ni Mambosasa. Sababu mojawapo ni

kwamba anaamini kuwa ndiye kielelezo cha mwanamapinduzi na mzalendo. Lakini matendo yake hayaoani na imani yake. Kwa ujumla, wahusika wote wawili wanajidunisha kutokana na matendo yao.

Baada ya kuhitimu katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, wanaajiriwa kazi ya ualimu lakini baada ya muda usio mrefu wanapigwa kalamu na kuadhibiwa na serikali kwa kufanya uhalifu mkubwa wa kunajisi na pia kumpiga mwalimu wa siasa wakiwa katika jeshi la kujenga taifa. Ukosefu wa nidhamu na unyama kama huu hauwezi kuhusishwa na uanamapinduzi wala usomi. Kwa kawaida wanamapimduzi huwa ni watu wenye nidhamu ya kiwango cha juu. Aidha, wasomi hutarajiwa kuwa waadilifu. Kutokana na udhaifu wao, Mambosasa na Mamboleo wanajitokeza kama watu duni wasio na uwezo wa kuyafikia yale wanayoyatamani. Tabia yao ya kiburi ndiyo inayoshambuliwa kitashtiti.

Adhabu ambayo Mamboleo na Mambosasa wanapewa na serikali ni agizo la kuishi vijijini kwa muda: "Waishi na watu vijijini ili wapate kuelewa ukweli wa mambo" (uk.61). Kauli hii inadokeza kwamba ijapokuwa wao ni wasomi, hawajui uhalisi wa maisha. Wakiwa kijijini, udhaifu wao unazidi kudhihirika kutokana na kushiriki kwao katika mambo ambayo ni ya kuchekesha na kuchukiza wakati mwingine. Kwanza, wanavunja matumaini ya wanakijiji. Katika kijiji cha Bucho, wao tu ndio wenye elimu ya chuo kikuu. Kwa sababu hii, wanakijiji wanawathamini sana na kujawa na matumaini kwamba wataenda mbali maishani na wataleta ustawi utakaowanufaisha wote. Hivyo, wanakijiji wanawachagua kuwa viongozi wao. Mambosasa anachaguliwa kuwa mwenyekiti, na Mamboleo anachaguliwa kuwa katibu. Lakini wanashindwa kuzitumia nyadhifa hizi kuleta mabadiliko ya kuwanufaisha wanakijiji. Mambosasa anatumia wadhifa wake kupora pesa za kijiji. Mamboleo anapomlaumu, anajitetea kwa njia ya kuchekesha. Anadai kuwa amekatishwa tamaa na viongozi wa juu serikalini, ambao ni wafisadi. "Inabidi nami nianze kuwa kama wao," anasema (uk.85). Hiki ni kisingizio cha kufichia uovu wake wa kushiriki katika ufisadi. Ni wazi kwamba uzandiki wake ndio unaopigwa vita hapa. Hatimaye, Mamboleo na Mambosasa wanaondolewa katika uongozi wa kijiji kwa kushindwa kuwajibika ipasavyo. Viongozi wapya wanachaguliwa, na ndio wanaoleta ustawi kijijini. Chini ya usimamizi bora wa Kamala, kijiji cha ujamaa cha Bucho kinaishia kuwa kijiji bora zaidi wilayani (uk.112). Uongozi wa wasomi unagotanishwa na ule wa mwanakijiji wa kawaida, yaani Kamala, ili kuubeza na kutilia mkazo ulivyoshindwa. [2]

---

[2] Wamitila (2003:213) anaieleza mbinu ya kugotanisha au "tajawuri" kama "mbinu ya uwekaji sambamba matukio au maelezo…ili kukifanya kinachozungumziwa kijitokeze wazi…." Tafsiri yake ya Kiingereza ni *juxtaposition*.

Tukio mojawapo la kuchekesha zaidi ambapo Mamboleo na Mambosasa wanahusika ni makabiliano kati yao na Padri Madevu. Wanakwenda nyumbani kwake kumkemea kwa sababu ya mahubiri yake ambayo yanawapotosha wananchi. Majibizano makali kati yao na Padri Madevu yanadhihirisha tofauti kubwa za kiitikadi kati yao. Aidha, adui yao anaonyesha waziwazi jinsi anavyowadharau wao, serikali yao na siasa yao ya ujamaa. Hatimaye wanapigana. Padri Madevu anawapiga vibaya na kisha kuwapeleka hospitalini. Licha ya kuchekesha, tukio hili linazidi kuwadunisha Mamboleo na Mambosasa. Hivi ni kwa sababu (mbali na kuwabwaga) Padri Madevu anadhihirisha kuwa ufahamu wao wa ujamaa, historia na uchumi ni mdogo. Hivi ni kusema kuwa Padri Madevu anawakomoa barabara.

Ijapokuwa Mambosasa na Mamboleo wanashabihiana kwa mambo mengi, bado wanatofautiana kimawazo na kitabia. Mbinu za kitashtiti zimetumiwa kubainisha tofauti hizi na hatimaye kumsawiri Mambosasa kama kiumbe duni kuliko Mamboleo. Tofauti mojawapo ni kuwa Mamboleo hutumia muda mwingi akiitathmini siasa ya ujamaa na utekelezaji wa sera zake. Mara kwa mara anaukosoa ujamaa na kutoa maoni yake kwamba unaweza kushindwa. Kwa mfano siku moja akizungumza na Mambosasa anasema: “Naona siasa yetu ya ujamaa haitaweza kufanikiwa…” Mambosasa anamjibu: “Tangu zamani nilihisi wewe ni mpingamapinduzi” (uk.83). Katika mazungumzo kama haya, Mambosasa anajitokeza kama aliyeleweshwa na siasa. Anazikubali sera za ujamaa bila kuzihakiki kama ilivyo wajibu wa msomi kufanya. Kwa jumla, mawazo yake ni ya kiudhanifu sana na yasiyotilia maanani uhalisi wa maisha.

Ni kutokana na tabia hii ya kupurukusha ukweli ambapo anakuwa na ndoto ya kwamba karibuni atachaguliwa kuwa mbunge na ataishia kuwa waziri. Anamwambia mkewe: “…ubunge nitagombea. Na utaona nitakuwa mbunge! Ikiwezekana hata uwaziri nitapata. Mawaziri wangapi nchini wamehitimu Chuo Kikuu….” (uk.94). Anachukulia kwamba kuhitimu chuo kikuu ni kama ufunguo utakaomfungulia mlango kuingia katika wadhifa wowote. Amesahau kwamba ameshindwa kusimamia shughuli za kijiji akiwa mwenyekiti mpaka akaondolewa na wananchi. Wale anaowaeleza juu ya ndoto yake (kama vile mkewe na rafikiye Mamboleo) wanamcheka kwa sababu wanajua ni ndoto ya kijinga. Mamboleo akiwa amerudishwa kazini na kumwacha Mambosasa kijijini, anamwandikia barua ya kumcheka kwa maneno yafuatayo: “Wewe chapa kazi kama kawaida. Usisumbuke na ubunge. Au labda umeupata?” Baadaye tunaelezwa kwamba hakuupata ubunge wala kukaribia kuupata. Hivyo ndivyo ujinga wa Mambosasa unavyobezwa.

Kilele cha kubezwa na kudunishwa kwa Mambosasa kinafikiwa anapojidanganya kwamba Rais Nyerere atakapoitembelea wilaya yake kukagua maendeleovijijini

ataweza kukutana naye. Lakini kama ilivyo kawaida ya shughuli rasmi kama ziara za rais, wanaoshiriki huwa wamealikwa. Mambosasa sio miongoni mwa wale walioalikwa kwa sababu sio mwenyekiti wa kijiji tena. Kwa hivyo hayumo kwenye ratiba ya sherehe. Kwa kuwa hataki kukubali ukweli huu, Mambosasa anajitayarisha na kwenda kwenye sherehe. Maelezo yanayotolewa kuhusu vitendo vyake katika kisa chote yamesheheni ucheshi lakini mara nyingine yanatufanya kumsikitikia mhusika huyu. Kwa mfano, anatembea umbali wa maili sita kwenda uwanja wa ndege ambapo Rais anatarajiwa kutua. Mwendo wote anasumbuliwa sana na wapanda baiskeli na waendeshaji magari ambao wanamtimulia vumbi na kuchafua mavazi yake. “Adhabu” hii inamfanya ayakumbuke na kuyawazia maovu aliyoyatenda siku za nyuma ambayo yamemtumbukiza katika hali duni aliyomo. Yaani, hali ya kuwa anatembea kwa miguu na hali watu wengine wanapanda baiskeli, kuendesha magari na hata kuruka kwa ndege. Tunaelezwa:

> Mawazo haya yalimsumbua sana kichwani kiasi cha wapanda baiskeli kumpigia kengele mara nyingi na kumtukana alipochelewa kuwapisha. Lakini mwishowe alianza kujilaumu mwenyewe. Alipokuwa Mwenyekiti wa kijiji, pesa nyingi zilipita na kutua mikononi mwake. Alianza kufikiri jinsi alivyozitumia ovyo; akajuta (uk.99).

Maelezo haya yanamdunisha Mambosasa kiasi cha kumfanya kiumbe wa kuhurumiwa, hasa anapojutia maovu yake. Kisa kinaendelea kusimulia jinsi Rais anapotua uwanja wa ndege, Mambosasa anapuuzwa na waandalizi wa sherehe kwa sababu hawamtambui. Baada ya sherehe fupi ya kumkaribisha kiongozi wa taifa, tangazo linatolewa kusema kwamba Rais ataondoka kwenda kwa gari kwenye uwanja wa sherehe hasa. Tunaelezwa jinsi Mambosasa anavyotumia hila ili awahi kwenye uwanja wa tafrija kwa maneno yafuatayo:

> Badala ya kujidai mtu mkubwa na mheshimiwa, alikata shauri kutenda matendo ya kiuanafunzi. Alikumbuka fujo zake za zamani pale Chuo Kikuu, jinsi alivyokuwa akiingia kwenye tafrija za walimu na kunywa kwa fujo na matusi juu ya walimu (uk.102).

Kwa kuongozwa na mawazo haya potofu, anadandia gari linalowapeleka wenyeviti wa vijiji. Wanapofika, Mambosasa anajipenyeza hadi kwenye ukumbi wa tafrija. Anapovuta kiti na kukaa, inachekesha sana anavyogunduliwa na askari wa kike wa jeshi la kujenga taifa ambaye anamwambia kwa ukali: “Wewe si mgeni! Tunaogopa tu kukufukuza mbele ya Rais. Kaa lakini usirudie tena safari nyingine!” (uk.103). Mambosasa anapopata fursa baadaye, anakunywa pombe na kulewa. Halafu la kuchekesha zaidi ni kwamba anapolewa, anakusanya makombo, kuyatia kwenye bahasha kubwa na kuyapelekea familia yake. Mkewe anamkaripia vikali na kuyatupa. Jambo linalozidisha bezo juu ya mhusika huyu ni jinsi alivyo kigeugeu.

Mara tunamuona akijutia makosa yake; lakini punde si punde anafanya mengine ambayo ni ya kitoto – kama tulivyoona hapo juu.

**3.0 Mama Tinda na Padri Madevu**

Tunawachunguza wahusika hawa kwa pamoja kwa sababu uumbaji wao kwa kutumia tashtiti unategemea uhusiano kati yao kwa kiwango kikubwa. Jambo hili litabainika katika maelezo yanayofuata. Mbinu ya kitashtiti inayotumiwa riwayani kumchora Mama Tinda ni ya ucheshi. Vitendo vyake anapoenda kanisani kuabudu vinaibua kicheko hasa kutokana na uelewa wake mdogo wa dini ya Kikristo. Jambo linalomsumbua mama huyu na linalomsukuma kwenda kanisani kumuomba Mungu amsaidie kukabiliana nalo linahusu tishio la kubomolewa kwa nyumba yake. Maofisa wanaotekeleza sera ya kuhamishia watu kwenye vijiji vipya wamemuonya kwamba nyumba yake iko nje ya kijiji kipya anachotakiwa kuhamia na kwa sababu hii itabomolewa. Analipinga sana jambo hili na hataki nyumba yake ibomolewe. Mama Tinda akiwa peke yake kanisani mkabala na sanamu za Yesu, Maria na kiwakilishi cha Utatu Mtakatifu, anaanza kwa kuikabili sanamu ya Yesu na kuomba ifuatavyo:

> Yesu! wewe ni Mungu. Ulizaliwa na mwanamke kama mimi. Mimi ni mama yako….Wewe uliyewachapa Wahindi kwa kuuza bidhaa zao ndani ya nyumba ya Baba yako, okoa nyumba zetu. Wachape hao watakaozibomoa (uk.2)

Ombi hili linachekesha kwa sababu ya mtindo wake usiokuwa wa kimaombi. Linajitokeza kama maelezo ambayo Mama Tinda anatoa kwa binadamu mwenzake. Pili, yanaonyesha kutoelewa mambo ya kimsingi kuhusiana na Ukristo, hasa kuzaliwa kwa Yesu na kitendo chake cha kuwafukuza hekaluni watu waliokuwa wakifanyia biashara humo.[3] Jambo la tatu ni kuwa Mama Tinda anawaombea adhabu maofisa waliomuonya juu ya nyumba yake kwa sababu anawachukulia kuwa watenda dhambi. Haelewi kwamba wanatekeleza sera mojawapo ya serikali kuhusiana na ujamaa. Anawaona tu kama watu waovu wanaotaka kumdhulumu.

Baada ya kuelekeza maombi yake kwa sanamu ya Yesu, Mama Tinda anaigeukia picha inayowakilisha Utatu Mtakatifu. Maelezo ya kitendo chake ni ya kuchekesha hata kuliko cha kwanza kilichoelezwa hapo juu. Tunaambiwa kwamba aliingiwa na wasiwasi kwa sababu mchoro huo ulimkumbusha mazimwi hatari ya ngano alizosimuliwa na bibi yake alipokuwa mtoto. Anaanza kujiuliza kama anakabiliana

---

[3] Kuhusu Yesu kuwafukuza wafanyibiashara kutoka hekaluni, imeelezwa katika Biblia – Mako 11:15-17 kwamba aliwashutumu waliohusika kwa kuifanya nyumba ya sala kuwa "pango la wanyang'anyi." Haikutajwa watu hao ni wa jamii gani lakini yamkini walikuwa Wayahudi. Mama Tinda anapowaita Wahindi, anaimithilisha (bila kujua) Yerusalemu na miji ya Afrika Mashariki ambapo aghalabu biashara huhusishwa na Wahindi.

na zimwi au Mungu. Ni katika hali hii ambapo anaanza kuomba: “Macho matatu! Wewe unaona kila mahali. Wamulike hao wenye mioyo ya wivu. Wameze…” (uk.3). Anashindwa kuendelea kwa sababu anazidiwa na wasiwasi wa kutojua “alikuwa akisali kwa nani.” Mwisho anamgeukia Maria Bikira – mamake Yesu – na kuanza kuomba hivi: “Maria Bikira uliyekuwa bikira hata baada ya kuzaa…”

Haitoshi kusema tu kwamba maelezo haya ya kuchekesha sana ya vitendo na matamshi ya Mama Tinda yanadhihirisha kutofahamu vizuri dini ya Kikiristo na hivyo kuushambulia ujinga wake. Jambo linaloshambuliwa vikali zaidi ni ile hali ya Waafrika kuletewa utamaduni wa kigeni – ikiwemo dini ya Kikristo – na Wazungu na wao kuupokea hata bila kuuelewa vizuri. Waafrika, kwa mfano, walikuwa na dini zao lakini walizitupa na kufuata za wageni. Kuenezwa kwa utamaduni wa Wazungu huku ule wa Waafrika ukiteketezwa ilikuwa sehemu muhimu ya mchakato wa kutawaliwa kwao kikoloni. Inasikitisha kwamba hata baada ya uhuru, Waafrika bado wanang’ang’ania utamaduni wa Wazungu hata kama unawatatanisha. Kwa hivyo kuchanganyikiwa kwa Mama Tinda anapokabiliana na ishara za Ukristo ni kuchanganikiwa kwa Mwafrika kwa jumla.

Anayeongoza ibada katika kanisa lililotajwa hapo juu ni Padri Madevu. Asili ya jina hili la kimasihara ni lakabu ambayo alipewa na wanakijiji ambao walishindwa kutamka jina lake halisi, yaani Emptyhead. Licha ya kuwa la kimajazi, jina hili ni la kimzaha vile vile.[4] Ni jina la kimajazi kwa sababu tunapolitafsiri, maana yake inakuwa mtu mpumbavu. Katika muktadha wa kisiasa na kijamii unaohusika, Padri Madevu ni mpumbavu kwa sababu hatambui uzuri wa ujamaa na ndiyo sababu anawachochea wananchi kuukataa na kuiasi serikali yao. Sifa nyingine ya Padri Madevu ni kwamba ni mnafiki mkubwa ambaye anajifanya mtumishi wa Mungu huku akifanya uzinifu na wanawake wa kijijini. Ufasiki wake unadokezwa katika maelezo ya jinsi anavyoanza misa:

> Kabla ya kuanza misa Padri Madevu alitupia macho upande wa wanawake.
> ... kisha alimwona mwanamke mjane amekaa mbele. Tamaa mbaya ilimwingia.
> Aligeuza kichwa haraka na kutazama upande wa wanaume (uk.3)

Mmoja wa wanawake ambao Padri Madevu ana uhusiano wa kimapenzi nao ni Mama Tinda. Anamtembelea nyumbani kwake mama huyu mara kwa mara, kulala naye na kumpa zawadi mbalimbali. Mama Tinda anauthamini uhusiano huu kiasi kwamba bintiye anapolalamika kwamba majirani wanawasema vibaya, anamkemea na kujitetea akisema: “Bila yeye tungekula nini? Hujui kwamba ni Baraka ya

[4] Tunatumia istilahi ya majazi kurejelea jina ambalo linaakisi tabia au sifa muhimu za mhusika. Tafsiri yake ya Kiingereza ni *allegorical name*.

Mungu…." (uk.9) Ufasiki na uzandiki wa Padri Madevu ndio unaoshambuliwa kwa bezo na maelezo haya.

Mbali na mbinu za kitashtiti za ucheshi, bezo na majazi zilizotumiwa kumchora Padri Madevu, pia kuna matumizi ya kinaya cha hali. Hivi ni kwa sababu kwa kawaida, padre ni mtumishi wa Mungu na pia kiongozi wa kidini ambaye anatarajiwa kuwa mwadilifu na mnyofu. Lakini tabia na mienendo yake ni kinyume cha matarajio haya. Mbali na sifa zilizotajwa hapo juu, mhusika huyu ni mdanganyifu mkubwa na tisho kwa uthabiti wa nchi. Inakuja kugunduliwa hatimaye kwamba Emptyhead sio padre bali jasusi wa shirika la upelelezi la CIA. Kazi yake hasa ilikuwa ni kuvuruga ujamaa nchini Tanzania kwa niaba ya serikali ya Marekani ambayo ilichukia siasa za aina hii kwa sababu ilizihusisha na ukomunisti.

Mfano mwingine wa kinaya cha hali unahusiana na vifo vya Padri Madevu na mpenzi wake Mama Tinda. Mambosasa ndiye anayepanga kifo cha Padri Madevu ambaye ni adui yake mkubwa. Anamtumia mpenzi wake na baadaye mke wake, Tinda, kutekeleza mpango huu ambao unahusu kumtilia Padri Madevu sumu katika chakula. Mpango wa mauaji unatekelezwa Padre Madevu anapomtembelea Mama Tinda nyumbani kwake – kama kawaida. Kwa bahati mbaya, mamake Tinda pia anakula chakula ambacho kilidhamiriwa kuliwa na Padri Madevu peke yake. Kesho yake, wote wawili wanakutwa wakiwa wamekufa. Tunaelezwa ifuatavyo: "Mama Tinda na Padri Madevu walikuwa wamekauka hali wamekumbatiana. Ilikuwa aibu ya mwaka" (uk.81). Hivyo ndivyo Tinda anavyosababisha kifo cha mamake bila kudhamiria.

**4.0 Mzee Chilongo**

Mhusika huyu ni kiwakilishi cha Watanzania ambao wamedhibitiwa na utamaduni wa kijadi kiasi kwamba hawataki mabadiliko na kwa hivyo wanapinga ujamaa ambao unahusishwa na ujenzi wa jamii mpya. Vitendo na matamshi yake yamewasilishwa kwa ucheshi mkubwa kwa hivyo ni ya kusisimua na wakati huo huo kuufichua udhaifu wa mhusika huyu. Sifa kuu ya Mzee Chilongo ni kuchukia kwake mabadiliko na kujitolea kwake kupigana nayo. Lakini jitihada zake zinachekesha kwa sababu ni wazi kwamba katika muktadha wa riwayani haziwezi kufaulu. Mbinu kadha za kitashtiti zimetumiwa kuushambulia uhafidhina wake.

Mfano mmoja wa jitihada za Mzee Chilongo kupigana na mabadiliko unahusiana na tukio la wanakijiji wa Kisole kuamua kukataa kuhamishiwa kwenye kijiji kipya. Hivyo, wanaume wote wanajificha porini ili kupambana na wanamgambo wa serikali wanaokuja kuwahamisha. Mzee Chilongo ni mmojawapo wa wanaume wanaowashambulia wanamgambo. Anajitokeza kuwa hodari katika matumizi ya

silaha za kiasili kama vile uta na mishale. Baada ya mapambano, anawaeleza wenzake jinsi alivyomfuma mshale mwanamgambo:

> Nilimshika vizuri 'sina-huruma' jina la mshale wangu, kisha nikavuta. nikalenga barabara sikio la kongoni wangu mnono. Nilipouacha, mshale ulikwenda kama upepo, nao haukuvunja ahadi yake. Ulitua vizuri pale pale nilipoutuma, ukaziba lile tundu lenye kiburi lililokataa kusikia kilio chetu. Mara moja nilimwona huyo kongoni anarukaruka kama beberu lililonusa matako ya mbuzi jike (uk. 30).

Ucheshi wa kifungu hiki umerutubishwa na mbinu nyingine kadha za kimtindo ambazo zinaleta athari ya msisitizo na udhahiri (*vividness*). Kwa mfano, kuna tashihisi inayotokana na Mzee Chilongo kuuzungumzia mshale wake kana kwamba ni binadamu. Sikio pia linahuishwa kwa kurejelewa kama lenye kiburi. Pia kuna sitiari inayotokana na ulinganishaji wa mwanamgambo na korongo mnono. Hii inaleta picha ya windo lenye thamani kubwa. Kadhalika, kuna tashibihi ya kuchekesha mwishoni ambapo athari ya windo kufumwa na mshale sikioni inamithilishwa na afanyavyo beberu anaponusa sehemu za uzazi za mbuzi jike. Mifano hii inathibitisha kwamba mtindo wa kitashtiti unaweza kufanikishwa na matumizi ya mbinu nyingi kuliko zile ambazo kwa kawaida zinahusishwa na mtindo huu, hasa ucheshi, kinaya, chuku na tabaini.

Jitihada za Mzee Chilongo na wapiganaji wengine wa Kisole ni kazi bure na za kuchekesha kwa sababu serikali inajibu uchokozi wao kwa kuwatumia kikosi cha askari wenye bunduki kuwatia adabu. Mzee Chilongo anazidi kuchekesha kwa jinsi anavyokaidi agizo la askari la kuinua mikono huku wenzake wote wanatii. Anamjibu askari kwa ujeuri: "Mimi siinui mikono juu kubeba mzigo nisiouona!" Anaishia kupigwa buti la kichwani na kuzimia. Askari wanampeleka hospitalini huku wenzake wakipelekwa kwenye boma la Mkuu wa Wilaya ambapo wanaadhibiwa na kufanyiwa dhihaka chungu nzima. Tunaona matumizi ya kinaya cha kiusemi Mkuu wa Wilaya anapowarejelea waliokamatwa kama "Mashujaa wa Tanzania". Hiki ni kinyume cha ukweli kwa sababu wangekuwa mashujaa wasingekuwa bomani wakiadhibiwa. Kwa hivyo hii ni kauli ya kuwacheka kwa ujinga wao wa kujaribu kupigana na serikali.

Ukaidi na uhafidhina wa Mzee Chilongo unazidi kushambuliwa kitashtiti akiwa amelazwa hospitalini. Anayapeleka huko mazoea yake ya kuwatusi na kuwapiga wanawake. Ndiyo sababu anamtusi mwuguzi anayesafisha vidonda vya wagonjwa. Kisha anampiga kwa gongo lake na kumuumiza. Mwuguzi anaanguka na kuzimia. Tunaelezwa kwamba Mzee Chilongo anakataa kuomba msamaha "kwa kitendo ambacho alikuwa amezoea kufanya nyumbani" (uk.45). Ni kitendo kinachofichua alivyojawa na taasubi.

Mzee Chilongo pia anajitokeza kama mwenye mawazo yaliyopitwa na wakati kwa jinsi anavyopinga matumizi ya maji ya bomba baada ya kuzinduliwa kwake katika kijiji cha Kisole. Kufuatia maendeleo haya, kunatolewa agizo la watu wote kukoma kuogea mitoni na visimani na kuanza kuogea uani. Lakini Mzee Chilongo anaona kwamba badiliko hili litashusha hadhi yake kama mwanamume. Anasema:

> Nataka kuogea mtoni kwenye maji yatembeayo. Mtoni kwenye samaki na nyoka! Nataka kukoga ziwani kwenye mamba! Mimi sijawa mzee kiasi cha kuletewa maji ya kukoga uani! (uk.123)

Anayatamka maneno haya mbele ya wake zake ili kuonyesha udume wake. Masimulizi ya riwayani yanafikia mwisho kwa kuelezea jinsi uhafidhina wa Mzee Chilongo unavyomtumbukiza katika upweke. Kwa sababu amekataa kusonga mbele kimaendeleo pamoja na watu wengine, anabaki nyuma peke yake katika mienendo ya kizamani ambayo haina nafasi katika Tanzania mpya. Hivyo, anapokwenda mtoni kuoga akitarajia kwamba atakutana na wanakijiji wengine, anajikuta peke yake. Hapa ndipo anapochorwa kama kiumbe duni wa kusikitikiwa. Kilele cha matumizi ya ucheshi na bezo kumchora mhusika huyu kinafikiwa anaposhtuka kumuona nyoka mkubwa kwenye miti kando ya mto anamoogelea. Anaokota mawe na kumpiga lakini baadaye anagundua kwamba hamna nyoka bali gamba lake lililokauka. Mzee Chilongo anajicheka mwenyewe kwa kuingiwa na hofu bure. Gamba la nyoka imetumiwa kama ishara ya jamii ya zamani. Jamii hii ni kama mabaki yaliyotokana na kujibambua kwa jamii ya sasa. Ujinga wa Mzee Chilongo kubaki katika jamii ya zamani ndio unaoshambuliwa kitashtiti.

**5.0 Hitimisho**

*Gamba la Nyoka* ni riwaya ya kitashtiti kwa maana ya kwamba imetumia mbinu kadha za utunzi ambazo kwa kawaida huhusishwa na mtindo wa tashtiti. Mbinu hizo ni kama vile ucheshi, bezo, dhihaka na kinaya cha aina mbalimbali. Tumeona pia kuwa kuna mbinu nyingine nyingi ambazo zimetumiwa kufanikisha mtindo wa kitashtiti riwayani. Mbinu hizo ni kama vile majazi, ishara, sitiari na tashibihi. Mtindo wa kitashtiti umetumiwa kuwaumba wahusika wakuu ambao ni Mamboleo, Mambosasa, Padri Madevu, Mama Tinda na Mzee Chilongo. Udhaifu wa kitabia wa wahusika hawa na maovu wanayohusishwa nayo umefichuliwa na kushambuliwa kitashtiti. Kwa kufanya hivyo, riwaya inayohusika imetoa mchango muhimu katika kurekebisha tabia, kutetea utu na kuitakasa jamii kutokana na maovu mbalimbali sio tu Tanzania lakini popote. Mtindo wa kitashtiti pia umefanikisha umbuji wa riwaya hii na kuifanya kuwa sanaa ya kiwango cha juu.

## Marejeleo

Abrams, M.H. (2005). *A Glossary of Literary Terms*. Boston: Thomas Wordsworth.
Baldick, C. (2001). *Oxford Dictionary of Literary Terms*. New York : Oxford University Press.
*Biblia: Habari Njema kwa Watu Wote* (1995). Dodoma: the Bible Society of Tanzania na Nairobi: The Bible Society of Kenya.
Boulton, M. (1975). *The Anatomy of the Novel*. London: Routledge and Kegan Paul.
Cuddon, J.A. (1999). *Literary Terms and Literary Theory*. London: Penguin Books.
Howthorn, J. (2010). *Studying the Novel*. London: Bloomsbury Academic.
Kezilahabi, E. (2006). *Gamba la Nyoka*. Nairobi: Vide-Muwa Publishers.
Mbatiah, M. (2001). *Kamusi ya Fasihi*. Nairobi: Standard Textbooks Graphics and Publishing.
*Mulika* (1984) Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.
Wamitila, K.W. (2003). *Kamusi ya Fasishi: Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Books.